

Ulaji>> Wastani wa kula nyama kwa kila Mtanzania ni kilo 15 kwa mwaka

Halmashauri zinazoendesha ufugaji nchini zaagizwa kujenga machinjio ya kimkakati

Na MWANDISHI WETU

HALMASHAURI zinazofanya shughuli za ufugaji nchini zimetakiwa kujenga machinjio ya kimkakati ili kupanua fursa ya soko la nyama na kujiongozea mapato.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita, Jijini Dodoma, alipokutana na timu ya wataalamu kutoka Manispaa ya Ilala, waliofika kutembelea machinjio ya Dodoma, ili kujifunza namna yanavyoendesha.

Profesa Ole Gabriel, alisema itapendeza kama kila halmashauri ikawa na machinjio ya kisasa kwa kuwa yatasaidia kuongeza mapato ya halmashauri hizo na kuachana na kukimbizana kila siku na waendeshaji wa machinjio yaliyopo sasa, ambayo hayana viwango vinavyotakiwa.

"Niwaombe makatibu tawala wa mikoa waliangalie hili. Waone uwezekano wa kujenga machinjio ya kisasa, yatakayosaidia kuboresha mazingira ya biashara yatakayochagiza kuongezeka kwa mapato ya halmashauri," alisema.

Aliongeza kuwa sio lazima halmashauri zijenge machinjio zenyewe, zinaweza kuingia

ubia na sekta binafsi na wakajenga machinjio ya kisasa, wakawa wanauza nyama katika soko la ndani na nje ya nchi, kodi ya serikali ikawa inalipwa na wateja wakaendelea kupata huduma nzuri.

Profesa Ole Gabriel, alisema biashara ya nyama sio ndogo huku akifafanua kuwa, kwa sasa wastani wa kilo milioni 2.6, za nyama zinaliwa nchini kila siku, hivyo aliwahimiza maafisa biashara kuelimisha jamii kuhusu zao la nyama ili watu wale nyama kwa wingi.

"Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), mahitaji ya kidunia kwa mtu mmoja anatakiwa kula kilo 50, kwa mwaka, lakini sisi Watanzania bado wastani wetu wa kula nyama kwa mtu bado upo chini sana, kwa sasa tumefikia kilo 15, kwa mwaka, bado kiasi ni kidogo sana," alieleza.

Aliongeza: "Maafisa biashara tumieni taaluma zenu kuelimisha umma kuhusu zao la nyama ili watu wale nyama. Watu wakila nyama kwa wingi, itachagiza biashara ya machinjio na ndipo hasa uwekezaji pia utakwenda vizuri."

Aidha, alipongeza Halmashauri ya Bahi kwa jitihada wanazoendelea nazo za kujenga machinjio ya kisasa, jambo ambalo litaboresha biashara ya machinjio na kuongeza pato la halmashauri hiyo.

Akieleza kuhusu machinjio ya Dodoma,

Profesa Ole Gabriel, alisema kabla machinjio hayo hayajachukuliwa na serikali, ng'ombe waliokuwa wanachinjwa kwa siku ni kati ya 40 mpaka 50, lakini tangu yarudishwe serikalini, namba ya ng'ombe wanaochinjwa imepanda kufikia 150.

"Mikakati tuliyonayo kuhusu machinjio ya Dodoma ni kuendelea kuiboresha kufikia kuwa machinjio ya mfano kwa Afrika Mashariki, ukanda wa nchi za SADC na hata ikiwezekana Afrika," alisema.

Profesa Ole Gabriel, aliwahakikishia wataalamu hao kuwa wizara ipo tayari kushirikiana na Manispaa ya Ilala, kuhakikisha mipango yao inafanikiwa na machinjio hayo yaweze kufanyakazi zake kama waliyokusudia.

Ofisa Masoko wa Manispaa ya Ilala, ambaye pia ndiye alikuwa kiongozi wa timu hiyo ya wataalamu, Ando Mwankuga, alisema machinjio ya Ilala ni mradi wa kimkakati katika kuboresha mazingira ya biashara ya machinjio, ambayo itakuwa na nyama za viwango zitakazouzika hata nje ya nchi.

"Lengo la mradi ni kuongeza mapato ya manispaa. Tunaamini mradi huu mkubwa, ambao utakuwa unachinja ng'ombe 1,500 na mbuzi 1,000, kila siku ukikamilika na kuanza kazi Desemba, mwaka huu, tutapunguza utegemezi kwa serikali," alisema.

PIKANO